
# THE SACRED NAME BROADCASTER

## Mtangazaji wa Jina Takatifu



5/2025

*a publication of* ***Assemblies of Yahweh***

THE SACRED NAME BROADCASTER

An **Assemblies of Yahweh** publication.
***Assemblies of Yahweh**, The **Narrow Way Newsletter**, **The Sacred Name Broadcaster**, **The Sacred Name Broadcast**, **The Sacred Scriptures**, **The Sacred Name Telecast**, and **WMLK Radio** are Service Marks and Trademarks of Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507*

***May 2025***
***Volume LVII, Number 2***

# YALIYOMO




***1 Kofia na Gauni ya Kuhitimu***

*Hebu tuangalie kwa makini sherehe za mahafali na tuelewe zilianzia wapi.*


***10 Messiah katika Agano la Kale, sehemu ya 7***

*Fundisho la Agano Jipya la Messiah linathibitishwa kutoka kwa mafundisho ya Agano la Kale, ambayo yanaunda msingi wa Imani yetu.*

***17 Viumbe Vya Yahweh Vilivyoumbwa, sehemu ya 7***

*Mwenye-nguvu Yahweh aliumba madarasa manne ya viumbe kumtumikia Yeye. Basi tuhakikishe kwamba hatulegei kamwe katika kujitolea kwetu kama walivyofanya wengine.*




Mtangazaji wa Jina Takatifu huchapishwa kila mwezi na Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507. Uandikishaji wako umelipwa na watendakazi wenzi wenye hiari wa huduma hii ambao wanajali kwamba ujumbe huu wa wokovu unapaswa kutolewa bila malipo kwa ulimwengu wote kama shahidi kabla ya Ujio wa Pili wa Yahshua Masihi. Ingawa hakuna malipo yoyote yatakayotozwa kwenye chapisho hili, MICHANGO (yote inakatwa kodi) inakubaliwa kwa shukrani ili kusaidia kulipia gharama. Tunatumahi kuwa utashiriki katika kufanya habari hii ipatikane kwa wengine.

Nukuu zote katika The Sacred Name Broadcaster zimetolewa kwa The Sacred Scriptures, Bethel Edition, 1981, Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507, isipokuwa ikitangazwa vingenevyo. Tafsiri zote za Biblia humu, zimesahihishwa ziwe thabiti na maandishi yaliyo ya awali zaidi yanayopatikana. Nakala za The Sacred Scriptures, Bethl Edition, zinapatikana. Kwa ujumbe jinsi ya kununua kopi yako, andika kwa Assemblies of Yahweh.

© Hakimiliki 2024 Assemblies of Yahweh. Haki zote zimehifadhiwa.
Malipo ya posta ya mara kwa mara huko Reading, PA 19612 (ISSN 879320). Simu (717) 933-4518. POSTA: Tuma fomu 3579 kwa Assemblies of Yahweh, SLP C, Bethel, PA 19507.


***Mwanzilishi na Mwandishi:** Mzee Jacob O. Meyer*

## Jalada Letu

***"Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani laki halinyauki ; na kila alitendalo litafanikiwa."** (Zaburi 1:3)*

*Mti wa mzeituni ni kitovu cha picha ya jalada mwezi huu. Mti wa mzeituni ulikuwa mazao muhimu kwa Israeli chini kupitia zama, ukitoa mafuta kwa kupikia na kwa mwanga, vile vile kwa kuliwa.*

*Mti wa mzeituni hauangushi matawi yake kila msimu wa majani kupukutika- unabakia kijani kila wakati. **"Bali mimi ni kama mzeituni umeao katika nyumba ya Elohim: Nazitumainia fadhili za Elohim milele na milele."** (Zaburi 52:8).*




*Mti wa mizeituni hauanzi kuzaa mpaka unapokaribia miaka 40 na unabaki ukizaa matunda kwa miaka 1,000 au zaidi. Tunataka kuiga mti wa mzeituni kuzaa matunda hadi uzeeni.*

*Zaburi ya sabato, Zaburi 92, inazungumzia kwa hamu yetu kuwa washiriki wenye tija wa ibada ya Kweli- kama wazee na manabii wa zamani- bado wakizaa matunda ya haki kwa miongo. **"Waliopandwa katika nyumba ya Elohim; watasitawi katika nyua za Elohim wetu. Watazaaa matunda hadi wakati wa uzee, watajaa utomvu, watakuwa na ubichi. Watangaze ya kuwa Yahweh ni mwenye adili, mwamba wangu, ndani yake hamna udhalimu."** (Zaburi 92:13-15).*



# Kofia & Gauni

## YA KUHITIMU

Na Mzee Jacob O. Meyer

Mfalme Suleimani kwa maneno yenye nguvu, aliwahimiza waumini wa Kweli kutafuta hekima, maarifa, na ufahamu.

***"Mithali za Suleimani, mwana wa Daudi, Mfalme wa Israeli. Kujua hekima na adabu; kutambua maneno ya ufahamu; kufundishwa matendo ya busara, katika haki na hukumu na adili. Kuwapa wajinga werevu, na kijana maarifa na hadhari; mwenye hekima asikie na kuongezewa elimu, na mwenye ufahamu ayafikie mashauri yenye njia. Kufahamu mithali na kitendawili, na maneno ya wenye hekima na mafumbo yao. Kumcha Yahweh ni chanzo cha maarifa, bali wapumbuvu hudharau hekima na adabu."*** (Mithali 1:1-7).

Suleimani aliimarisha ushauri huu kutii Neno la Yahweh katika mlango wa pili wa Mithali.



***Laureli takatifu (iliyoonyeshwa kwenye shada, au duara) inashikiliwa juu na Nike, ushindi wenye mabawa, kumtawaza Zeus kama mshindi.***

***"Mwanangu, kama ukiyakubali maneno yangu, na kuyaweka akiba maagizo yangu. Hata ukatega sikio lako kusikia hekima, ukauelekeza moyo wako upate kufahamu; Naam, ukiita busara, na kupaza sauti yako upate ufahamu; ukiutafuta kama fedha, na kuutafuta kama hazina iliyositirika; ndipo utakapofahamu kumcha Yahweh, na kupata kumjua Yahweh. Kwa kuwa Yahweh huwapa watu hekima; kinywani mwake hutoka maarifa na ufahamu; huwawekea wanyofu akiba ya hekima kamili; yeye ni ngao kwao waendao kwa ukamilifu; Apate kuyalinda mapito ya hukumu, na kuhifadhi njia ya watakatifu wake. Ndipo utakapofahamu haki na hukumu, na adili, na kila njia njema. Maana hekima itaingia moyoni mwako, na maarifa yatakupendeza nafsi yako; busara itakulinda; ufahamu utakuhifadhi. Ili kukuokoa na njia ya uovu, na watu wanenao yaliyopotoka; na watu waziachao njia za unyofu, ili kuzienda njia za giza; Wafurahio kutenda mabaya; wapendezwao na upoteo wa waovu; waliopotoka katika njia zao, walio wakaidi katika mapito yao. Ili kuokoa na malaya, Naam, malaya mwenye kubembeleza kwa maneno yake; Amwachaye rafiki wa ujana wake, na kulisahau agano la Elohim wake."*** (Mithali 2:1-17).

Assemblies of Yahweh kila mara imehamasisha kutafuta kwa hekima na maarifa. Tunaamini kwamba hekima ya kibiblia inajenga nyumba ya kiroho ya waumini. Elimu katika mafundisho ya kibiblia inaendeleza muundo wenye nguvu wa kiroho ulio juu ya nguzo saba za ufahamu, Mithali 9:1. Ni ya kuvutia kubaini kwamba kitabu cha Mithali kinaonekana kuwa kilichogawanywa kwenye sehemu saba. Pengine katika njia hii, Suleimani alitafuta kusisitiza umuhimu wa nini aliyofundisha.

Hata hivyyo, kutoka kwa miaka yetu ya uchunguzi wa karibu inakuwa dhahiri kwamba hekima ya Yahweh iliyopo katika Maandiko yaliyoongozwa, inapita kwa mbali hekima ya ulimwengu huu. Kwa mfano, dunia imeanzisha mfumo wa kielimu, unaonekana tofauti na yale Mwenye-nguvu Yahweh ameainisha wazi katika Maandiko. Katika njia mingi, ulimwengu wa

kitaalamu umetafuta utafutaji wa hekima ulioanzishwa na Mwenye-nguvu Yahweh. Walakini, katika njia zingine, mfumo wa kielimu wa ulimwengu unaonekana kudumisha mila za upagani wa kale. Hakika, watu wachache wa ulimwengu wamefuata kanuni za kusoma zilizoanzishwa katika Mithali 1 na Zaburi 1.

Wakati mwanafunzi, katika mfumo wa kielimu wa kidunia anatimiza mahitaji fulani ya ujumuishaji, anafikia shahada ya juu bila kujali kwa kiwango chake cha maarifa. Maandiko Matakatifu hayaungi mkono dhana ya kujitahidi tu kwa sifa ya digrii, lakini kwamba zawadi yetu kwa kusoma kwa bidii kwa Biblia kutaweza, hatimaye, kukubaliwa kwenye familia ya Aliye Juu katika Kuja Mara ya Pili kwa Yahshua aliye Messiah. Wakati ulimwengu unatunukia kwa wanafunzi shahada mbalimbali za kitaaluma kutambua kiwango chao cha maendeleo ya kielimu, historia inaonyesha kwamba mfumo kama huo umewekwa kimsingi juu ya mila za kale za upagani.

Moja ya kiwango cha hatua kilichoundwa na mfumo wa kidunia wa elimu, kinatokea katika kuhitimu, au zoezi la kuanza. Kuweka alama kupita kwa degrii iliyoteuliwa ya kufanikiwa kwa kusoma, sherehe adhimu zinafanywa ambazo zinachukua aina fulani ya gwaride.

Inayojitokeza katika sherehe ya kuhitimu, au kuanza ni maandamano NA WASHIRIKI WAKIVAA MAVAZI YA KITAALUMA.Wahitimu- kawaida wakivalia kofia na gauni. Mtu wa wastani bila shaka anakubali sherehe hizi na haonekani kuelewa mila hatari za upagani ambazo zimefichwa chini ya sherehe hizi za kimila. Mara nyingi matarajio ya mwanafunzi ya kufanikiwa katika kushiriki katika sherehe kama hizo yanazidi hamu ya kumtumikia Mwenye-nguvu Yahweh na kuepuka uchafuzi wa mfumo huu wa kidunia.

Ruhusu tuchukue mtazamo wa karibu kwa sherehe za kuhitimu na kuelewa ni wapi zilianzia. Kisha baada ya kuwa tumechunguza ukweli ambao tumeweza kufukua kutoka kwa utafiti wa kielimu, kila mmoja lazima afikie kwa hitimisho yake mwenyewe na kutumia maarifa kulingana kwa uwezo wake kwa kutii.

## Bachelor na Baccalaureate

Tunapochuguza moja ya maneno yaliyopewa digrii za kitaaluma, ukweli fulani wa kushangaza unajitokeza. Shahada ya kwanza kamili inayotolewa na taasisi ya kielimu ya sekondari inaitwa "Bachelor Degree (shahada ya kwanza)." Mtu kawaida anafikiria kuhusu *bachelor*, kama mtu ambaye hajaoa aliye na majukumu machache- ufafanuzi wa msingi katika kamusi fulani. Sasa swali linaibuka sababu kwa nini neno hili linapaswa kutumiwa kuonyesha degrii ya kitaaluma.

**Webster's New World Dictionary**, *Second College Edition*, inaelekeza muulizaji kwa neno "*baccalaurete*" kwa mazingatio zaidi. Entimolojia ya neno hili inasemekana kufuatilia kwa "laurel berry" kutoka kwa neno la Kilatini cha Kati *baccalaureatus*. Walakini, wanapendekeza kwamba linafuatilia kwa neno la Kilatini cha Kati kumaanisha "mkulima kibaraka, kijana mtukufu anayetafuta kuwa *knight* (*baccalaris*)." Wanapendekeza neno la Gaulish *bakalakos*, mfanyikazi, au mchungaji, ambalo wanadhania kufuatilia kwa mzizi wa Kilatin *baculum*- mfanyakazi."

Walakini, jambo la kushangaza sana ni dhahiri kupitia kwa muhtasari wa uwanja wa ushirika wa maneno katika **Oxford English Dictionary**. Kwa neno *bacchanal* maendelezo tofauti ni pamoja na *bacca* na *baca* kama viambishi awali. Neno *bacchanal* (mahali palipotolewa kwa *Bacchu*) linaunda msingi wa neno *Bacchanalia*- sikukuu ya *Bacchus*.

Kuhitimisha entimolojia hii imara zaidi, iliyojumuishwa na nakala hii ni uwakilishi wa kale wa aliye na nguvu huyu wa upagani wa Kigiriki na Kirumi ambaye ni wa furaha ya pombe. Ni wazi, mtu anaweza kumtambua huyu aliye na nguvu, mwenyewe pamoja na waabudu wake wakionyeshwa na yeye, kama waliovalia shada la maua kama taji kuzunguka vichwa vyao- laurel ya Bacchus (baccalaureate).

Kuvutia,Laurel takatifu (ikionyeshwa katika shada, au duara) inashikiliwa juu na Nike, ushindi wenye mabawa, kumtawaza Zeus kama mshindi (rejelea kwa Wanikolai, Ufunuo 2:6, 15). Katika kitabu, **The Two Babylons**, kilichoandikwa na Alexander Hislop, anafuatilia jina Bacchus kwa Dionysus na, mwishowe, kwa Zeus (uk. 72). Hislop anaelezea kwamba Bacchus, au Dionysus, ilimaanisha *anayebeba dhambi* kama jina la

***Sanamu ya Kirumi inayoonyesha Bacchus au Dionysus, m-ngu wa divai.***



*Zeus soter* (Mwokozi). Vikombe vingi bado vinaonyesha Nike akiwa na mabawa, akishikilia shada la maua juu kumtawaza mshindi.

Kunayo zaidi hapa kuliko yanayokutana na macho. Uhusiano wa karibu wa majina unakuwa dhahiri kupitia tafakari. Bacchus hakuwa tu mwenye nguvu ambaye uabudu wake ulijumuisha karamu za ulevi na tafrija (kama katika New Orleans Mardi Gras). Ibada yake imeunganishwa kwenye sherehe kubwa za Ukr-sto, Krsmasi, pamoja na Easter, wakati mwingine anaonyeshwa akiwa na kitambaa cha kichwa (baini marejeleo kwa *tippet* baadaye katika nakala hii) ambayo ilipambwa misalamba mingi. (Yahshua aliye Messiah hakuuawa juu ya msalaba, lakini juu ya mti, au mti wa mateso. Umeweza kusoma nakala yetu juu ya mada hii? Ni bure kwa anayeulizia.)

Pengine, hii ndiyo sababu kwa nini unywaji wa pombe kupita kiasi, mara nyingi unaandamana na siku za mwisho za maisha ya chuo kikuu ya mwanfunzi, kabla tu ya kuhitimu. Kunao uhusiano hapa kwa ibada ya kale ya Bacchus na sherehe za ulevi kwa kuwa umeshinda ushindi wa kitaaluma? Mtu anaweza kubashiri tu.


Kwa nini ni muhimu kuhudhuria huduma ya kidini wakati darasa la wakubwa linahitimu kutoka shule ya upili au chuo kikuu? Je, haionekani ya kushangaza kwamba huduma kama hiyo ya baccalaureate inafanyika wakati hakuna maelezo kama hayo ya huduma yanaonekana, au kuamuriwa kuzingatiwa katika Maandiko Matakatifu? Ibada ya Mwenye-nguvu Yahweh kwa wazi inasimama kando kutoka kwa ibada ya mataifa. Angalia Warumi 2:1-15. Kwa mazoezi ya kawaida ya Ukr-sto ya kutakasa mila za upagani wa mitaa na kuziunganisha kwenye vitendo vya mafundisho ya Ukr-sto, hatupaswi kuwa wenye shaka kwa huduma za kidini ambazo zinafanana kwa karibu hivyo kwa ibada za kale za mataifa? Kunayo mengi tu zaidi kuliko tu kufanana kwa bahati kwa mazoea ya ibada ya Bacchus?

Ingeonekana hivyo! Nini kuhusu vazi linalohitajika kwa sherehe za baccalaureate na kuhitimu? Je, vitendo hivi pia vilianzishwa na wapagani wa kale?

## Ibada za Kuhitimu sio za Kibiblia

Kauli ya kufunua sana inapatikana katika **Encyclopedia Britannica**, *Eleventh Edition*, Juzuu 23, Uk. 413, chini ya mada ya "Robes." Ruhusu tuelewe ni wapi matumizi ya mavazi haya maalum yalianzia.

"*Hakuna utafiti wa kina hadi sasa umeweza kufanywa wa mavazi ya mapema ya kitaaluma ya Kiingereza kama inavyolinganishwa kwa vyuo vikuu vya bara- utafiti ambao unapaswa kurusha mwanga mwingi juu ya mada. Swali la kuudhi ni hilo la umbali gani nguo ya kitaaluma imetolewa kutoka kwa ya kikanisa. Anthony Wood anatazama, kwamba imetolewa kutoka kwa tunica talaris na cucullus wa Benedictines, kwa sasa haungepata uungwaji mkono sana; lakini waandishi wengi wanaonekana kuwa na wasiwasi usio wa lazima kufuatilia kila bidhaa ya mavazi ya kitaaluma kwa vazi fulani dhahiri la kikanisa. Wasomi wa zama za kati walikuwa bila shaka, karani, na iliwabidi kuvalia vazi la ukarani na tonsure. Lakini, ukweli kwamba hili lilikuwa tukio linaifanya ngumu kutofautisha kati ya mavazi ya kitaaluma na kikanisa, mashuhuri katika tukio la brasses na monuments zingine za mhitimu wa chuo kikuu na watukufu ambao pia walikuwa makuhani. Chanzo kingine cha ugumu ni tofauti ya majina kwa ambao sehemu tofauti za mavazi ya kitaaluma yanaitwa katika kanuni za chuo kikuu na mahali pengine, wakati mwingine kusababisha mkanganyiko usioweza kutenganishwa.*"


Wanafunzi wa zama za kati walivalia nguo za ukarani (za kidini) na tonsures (kunyoa sehemu ya kichwa kuiga makuhani wa sanamu).

Kama tunavyoweza kuona, imependekezwa kwa nguvu kwamba MAVAZI YA KITAALUMA YALIFAFANA NA MAVAZI YA KIKANISA. Tutafuatilia mwelekeo huu kwa kina zaidi katika uchunguzi wetu. Kama, iliyokatazwa katika Walawi 21:5, **NIV**), lazima kuna uhusiano fulani kati ya wasomi na kanisa.

Kuongezea, lazima ibainishwe kwamba nakala ya ensaiklopedia hii inaashiria zaidi kwamba mavazi ya kitaaluma katika mfumo wa kielimu wa Uingereza unafuatiliawa tu kwa nusu ya pili ya karne ya 14 (miaka ya 1300). Kutoka hapo, yanaonekana kufuatiliwa kwa University of Paris. Hata hivyo, haiwezekani kufuatilia historia ya kidunia ya gauni za kitaaluma zaidi kuliko karne ya 13 C.E.

Pia ni ya kuvutia kubaini kwamba mavazi tofauti ya kitaaluma yanawakilisha digrii mbalimbali za maendeleo ya kielimu. Kila gauni haswa, hood, kofia, zinawakilisha vyuo vikuu mbalimbali maalum, katika kuon-

gezea kwa maendeleo ya mvaliaji katika taaluma tofauti.

Kwa sasa, Universtiy of New York inadumisha itifaki inayoelezea mavazi yanayokubaliwa ya kitaaluma kwa kila shahada ya kieleimu. Kulingana kwa kazi maarufu za utafiti, ikiwa taasisi yoyote ingetaka kufanya maandamano ya kitaaluma, wanapaswa kuwasiliana na chuo hiki kikuu kwa mahitaji maalum ya kuvalia ambayo yanakubaliwa kote.

## Mavazi ya Kibiblia tofauti na ya Kidunia

Haijatambuliwa kwa upana, lakini Biblia inaelezea tofauti tofauti kati ya mavazi yaliyovaliwa na makuhani wa Yahweh na makuhani wa Baali. Taratibu maalum ya mavazi ya kufuata utaratibu kwa makuhani wa Yahweh yanaelezewa wazi katika Kutoka 28 na 29.

Makuhani wa Yahweh walielekezwa kuvalia nguo takatifu maalum sana. Maneno ya Kiebrania yanatafsiriwa kama ifuatavyo. Kutoka 28:4 inasoma: "**Na mavazi watakayoyafanya ni haya: kifuko cha kifuani, na naivera, na joho, na kanzu ya kazi ya urembo, na kilemba, na mshipi;nao watafanyia Haruni nduguyo, na wanawe mavazi matakatifu ili anitumikie katika ofisi ya ukuhani**." Nguo hizi zinazingatiwa kama mavazi takatifu, na yalielezewa katika Maandishi kama kuwa na rangi sana na kujumuisha mavazi rasmi yanayohitajika kwa huduma.

Naivera (**Strong's** #646) lilikuwa vazi ndogo lililoundwa kuwa na mawe mawili ya shohamu kwenye mabega ambayo yalichongwa majina ya makabila ya Israeli. Mawe haya yaliwekwa katika mpangilio na kufungwa kwenye mabega ya vazi hili la nje kama kumbukumbu mbele ya Yahweh.Kamba au mikufu ya dhahabu ilikuwa iambatanishwe kwa mipangilio na kushuka chini kutoka kwa mabega kuelekea kwa kwapa kama sare za kijeshi za kisasa. Naivera ilifanywa kwa kitani nzuri, ya rangi nyeupe.

Kifuko cha kifuani (Kiebrania- *choshen mishpat*) kilikuwa cha kuvaliwa juu ya naivera, na hiki kilikuwa chenye mawe ya dhamani ya Urim na Thummim. Mipangilio ya mawe katika kifuko cha kifuani ilikuwa kuwakilisha kibinafsi kila kabila la Israeli.


Vazi (*me'il*, **Strong's** #4598) lilivaliwa chini ya naivera. Ilitengenezwa kwa kitambaa cha bluu chenye mapambo. Chini ya vazi ilikuwa ivaliwe kanzu (*ketoneth*, **Strong's** # 3801) ya kitani nzuri. Kilemba kilikuwa vazi la kichwa. Kitani katika istilahi za kibiblia inamaanisha "kitambaa cheupe kisichotiwa rangi." Kuongezea,*britches* za kitani zilikuwa zivaliwe kama nguo za ndani ili kwamba wakati Haruni au vizazi vyake, wanafanya huduma za sadaka juu ya kizingo cha madhabahu, sehemu zao za siri hazingefunuliwa mbele ya kusanyiko.

Ni dhahiri kwamba wakati makuhani wa Yahweh wanahudumu katika ofisi ya wawakilishi wa kidunia wa kidini wa Yahweh, wangevalia vazi la nje nyeupe, naivera ikifunika vazi. Vazi hili lenye rangi lingeweza pengine kuwaweka kando kutoka kwa wengine wa kusanyiko wanaoabudu. Kwa kuongezea, makuhani wachanga walifanya kazi yao katika *ketoneth* nyeupe (kanzu) pekee.



*William Cecil akiongoza Court of Wards*
*Sheria za Malkia Elizabeth zilisisitiza uvaaji wa kofia na gauni kwa wote, na kofia na tabia za wale walio na haki ya kuvazivalia*

Makuhani wa Baali pia walivalia mavazi tofauti. Ungepata yameelezewa katika Sefania 1:4. ***"Nami nitaunyosha mkono wangu juu ya Yuda, na juu ya watu wote wakaao Yerusalemu; nami nitayakatilia mbali***



***Mwabudu wa Kweli anapaswa kuvalia moja ya hizi, au anapaswa kukataa kofia hii ya jadi kama cheo cha upagani hata ingawa anaweza kutoruhusiwa kushiriki katika sherehe za kuhitimu?***

***mabaki ya Baali, yasionekane mahali hapa, na hilo jina la Wakemari pamoja na makuhani."*** Mabaki ya Baali yaliitwa *chemarim* (**Strong's** # 3649), kwani hiki kilikuwa cheo cha makuhani wao wanaoongoza. Entimolojia mbalimbali za msingi kwa neno la mzizi *kamar* zinapendekeza kwamba linamaanisha amevaa vazi jeusi lililofungwa. Istilahi hii pia inatumika katika 2 Wafalme 23:5 na Hosea 10:5. Makuhani wa Yahweh waliitwa *kohenim*.

Kwa sababu hiyo, watumishi hao, wasomi, au watendaji wa serikali ambao kwa sasa wanajivisha katika vazi ndefu, nyeusi lililovungwa, hawafuati mila za kidini za kibiblia katika maagizo yaliyotolewa na Mwenye-nguvu Yahweh kwa makuhani Wake. Wanaendeleza vitendo vya ukuhani wa Baali!

Makuhani wa Baali walikuwa kimsingi makuhani wa ibada ya jua. Tutaona katika utafiti wetu unaoendelea kwamba ibada ya jua inaunda usuli wa msingi kwa mila za kidini na desturi za mfumo huu wa ulimwengu wa kibabeli. Hii ni kauli kali, lakini,hata hivyo, inawezakana kutoka kwa kazi mashuhuri za utafiti ambazo zinatumika kwa kawaida sana katika mfumo wa kielimu wa wakati wetu.

Kama tulivyoona tayari, vazi la kitaaluma linavyoonekana linalo uhusiano fulani wa ndani kwa vazi za kikanisa. Hili linaelezewa kwa urahisi. Katika nyakati za zama za kati, vilevile katika Misri na Babeli ya kale, ilikuwa makuhani ambao walisemwa kuwa watu walioelimishwa.

Kwa mfano, makuhani wa Aesculapius walihudumu kama madaktari wa mapema. Kwa hivyo, uhusiano kati ya viwanja hivi viwili (dini na elimu), katika historia ya kale, ni karibu isiyoweza kutenganishwa na isiyoweza kutambulika. Hivi ndivyo mavazi yao yalikuja kuwa yanayohusiana. Kwa kiwango fulani, sawasawa ni kweli leo.

## Vazi la Kitaaluma la Kichwa

Kwa kusoma kupitia milango ya 28 na 29, inakuwa dhahiri kwamba makuhani wa Yahweh walikuwa wametolewa kilemba cheupe kilichopambwa mapambo. Mfumo wa siku za kisasa wa kitaaluma unatumia mavazi ya kichwa mbalimbali ya ibada yanayovaliwa kutofautisha shahada tofauti. Kofia (*hood*) tofauti, au *cap*, huonyesha kila digrii.

**Encyclopedia Britannica**, *Eleventh Edition* (bibliografia sawa kama mbeleni) inayo yafuatayo kusema kuhusu vifuniko vya vichwa tofauti: *Kofia hiyo hapo awali ilivaliwa na wasomi wote, kama kila mtu, na bila shaka haikuwa na umuhimu wa kielimu. Wakati mwingine kofia pia ilivaliwa, kofia ikirushwa nyuma (karani wa Chauncers wa Oxenford katika uangazaji wa hati ya Elsmere, anavalia kofia ya skull nyekundu, na tippet ya tatu na hood, huku kofia ikianguka nyuma ingawa haikuwa kwenye mabega) lakini kofia ya wahitimu ilikuwa imeisha kutumika kufikia mwisho wa karne*



**Watumishi hao, wasomi, au watendaji wa serikali ambao kwa sasa wanajivisha katika vazi ndefu nyeusi iliyofungwa, hawafuati mila za kidini za kibiblia katika maagizo yaliyotolewa na Mwenye-nguvu Yahweh kwa makuhani Wake**

*ya 16, kofia za Shahada(bachelor) zilipaswa kupambwa kwa manyoya, ambayo tunajifunza kutoka kwa sheria ya de admission ad pelluram (1432) kuwa ilikuwa ya Mabwana na wakuu wanaweza kutumia hariri katika majira ya joto. Kulikuwa na hoods dhahiri ya angalau aina mbili kwa mabwana. Haijatatuliwa wakati rangi za kisasa za kofia zilipotokea, labda walifuata zile za kanzu za vitivo, lakini kuhusu haya sisi ni wasio na uhakika. Oxford Proctor bado anavaa miniver hood. Kofia ya kisasa ya Cambridge imehifadhi umbo la asili kwa karibu zaidi kuliko ile ya Oxford, ikiwa ni kofia na tippet pamoja, hood ina pembe za mraba. Tippet ambayo inaonekana kama sehemu ya vazi la awali la madaktari fulani, labda ilikuwa, kama tippet ya hakimu, awali kofia ya bega ikiwa sehemu ya vazi sawa na kofia. Clark na wengine wangeipata kutoka kwa almuce, lakini haionekani kuonyesha msingi wowote wa kufanya hivyo. Nafasi yake inaonekana kuchukuliwa na skafu iliyovaliwa na D.D.'s nk., nayo labda ilitengenezwa kutoka kwa kofia yenye liripipe ndefu kama vilemba iliyovaliwa kichwani au kama skafu mabegani. Inaonekana ni ya mbali sana kupata skafu kutoka kwa pendenti mbili za almuce."*

Kuvutia zaidi ni uchunguzi ufuatao kutoka kwa **Encyclopedia Britannica,** nakala sawa. *"Mavazi ya kitaaluma yalifanyiwa uchunguzi mwingi na kusahihishwa wakati wa Matengenezo ya kanisa, yakiongozwa na utimamu na usawa, mavazi ya kupita kiasi yakikandamizwa kwa ukali kama zamani lakini sio kwa athari kubwa. Barua ya Burleighs kwa vice chancellor wa Cambridge University (1585) na, kanuni kama hizo ziliwekwa kwa Oxford na sheria za Laud za 1633, maelezo zaidi yalishughulikiwa na amri ya 1770"*

Ni dhahiri kutoka kwa nukuu ya mwisho, kwamba kwa kiasili, kulikuwa na kutokubaliana fulani kuhusiana na vazi la kitaaluma, lakini serikali baadaye ilisanifisha kanuni. Inavyoonekana Malkia Elizabeth aliongoza katika kufanya tofauti hizi . Kofia na kanzu zilihitajika katika maandamano ya kitaaluma, kama zilivyo leo na hitaji kwa kuzivaa kwa hafla kama hiyo ikifanywa lazima.

## Mortarboard-Kofia ya mahafali

Nukuu ya kushangaza kutoka **Encyclopedia Britannica** inasema kama ifuatavyo: *"UTUKUFU, katika kazi za sanaa, ni neno la jumla la mng'ao wowote wa nuru unaoonekana kuzunguka mwili wa mtu mtakatifu, kama vile nimbus, halo, aureole, mandorla, au vesica piscis. Kusudi lake ni kuwakilisha tabia ya kiroho kupitia ishara ya nuru. Sanduku la jua lilitumiwa katika Misri ya kale kuashiria uhusiano mahususi wa kiumbe cha kimungu na jua. Katika sanaa ya Kigiriki na Kirumi jua-[*mungu*]- na wafalme huonekana wakiwa na taji ya miale. Kwa sababu ya asili yake ya kipagani, aina hii iliepukwa katika sanaa ya Kikristo ya mapema. Kufikia karne ya 5, hata hivyo, fomu ya umbo la diski nyuma ya kichwa, iliyoitwa nimbus au halo, ilikubaliwa kikamilifu. Hapo awali iliwekwa kwa ajili ya [*Messiah*] na bikira, nimbus ilitumiwa hivi karibuni kwa ajili ya watakatifu pia. Msalaba ndani ya nimbus pande zote ulitambulishwa na uwakilishi wa [*Messiah*] katika Zama za Kati. Nimbus ya pembetatu iliashiria Utatu. Kwa muda fulani, katika karne ya 5 WATU HAI WA UMAARUFU WALIWEKWA NA NIMBUS YA MRABA; KUMBUKUMBU YA DESTURI HII IMEHIFADHIWA*



**St. Benedict akionyeshwa akiwa na halo.**

*KATIKA MORTARBOARD YA KITAALUMA.*

*"Nimbus, na vilevile aureole, hupatikana pia katika sanaa ya kibudhaa ya India. Tarehe yao ya mapema zaidi ya kuonekana ni mwishoni mwa karne ya 3 B.C.E, na yaelekea mawazo haya yaliletwa India na wavamizi Wagiriki."*

Kofia maarufu kwa sasa ya *mortarboard* inayovaliwa wakati wa sherehe za mahafali ni wazi imetolewa kutoka kwa upagani wa kale. Inaonekana kama kwamba pembe nne zilikusudiwa kuwakilisha pembe nne za msalaba. Kazi hii iliyozingatiwa sana ya utafiti **Encyclopedia Britannica** imesema kwa wazi. Kofia ya mortarboard ya kitaaluma ilikuja chini kwetu kutoka kwa upagani-kutoka kwa ibada ya jua. Uamuzi wa mwisho sasa ni wako kufanya.

*Mortarboard* pia inao umuhimu fulani katika Free Masonry, kwa sababu **Encyclopedia Of Free Masonry** inaonyesha kwamba *kofia ya mahafali* inatumiwa kwa kusudi la ibada ya ujenzi. Ensaiklopedia hii inatumia sifa




**Uwakilishi wa Aristotle unamwonyesha yeye kama amevalia kofia ya mtu aliyeelimishwa wa Kigiriki, ambayo inaonekana kuwa kama yalmulke inayovaliwa kwa sasa na Wayahudi.**

kwa hali ya Nimrodi, kama kuwa mwashi asili- kulingana na wao, Nimrodi anaajiri waashi 40,000 kujenga Babeli (mnara) na Ninawi. Kumbuka katika Mwanzo 10:8-12 kwamba Nimrodi alikuwa mtoa hoja mkuu katika upinzani kwa Yahweh, na alikuwa mwanzilishi wa Babeli na Ninawi.


Uwakilishi wa Plato na Aristotle unawaonyesha wao kama wamevalia kofia ya mtu aliyeelimishwa wa Kigiriki, ambayo inaonekana kuwa kama *yalmulke* inayovaliwa kwa sasa na Wayahudi. Ni muhimu kubaini kwamba katika kitabu cha kihistoria cha apokrifa cha 2 Makabayo 4:11 tunapata nukuu ifuatayo: **“** *Aliziweka kando kanuni za kifalme haswa zilizowapendelea Wayahudi, zilizopatikana kupitia kwa Yohana, Baba yake Eupolemusi, ambaye aliendа katika misheni kwa Warumi kutengeneza urafiki wa uhusiano na muungano nao, na kufuta njia za kisheria za maisha, ALIANZISHA DESTURI MPYA KINYUME NA SHERIA. Kwa hiari alianzisha ukumbi wa michezo hapo chini ya kijiji, na KUFANYA VIJANA WAZURI ZAIDI KUFAA KOFIA YA KIGRIKI. Na kwa nguvu hiyo akaendelea kwa mitindo ya Kigriki na kuja kwa desturi geni kukapanda, kwa sababu ya kuzidi kwa uovu kwa Jason [*mwenye dhambi*], ambaye hakuwa kuhani hata kidogo, kwamba makuhani hawakuwa wenye bidii tena kwa ajili ya utumishi wa madhabahu, bali wakidharau patakatifu na kupuuza dhabihu, walifanya haraka kushiriki katika mazoezi yasiyo halali katika shule ya mieleka, baada ya wito wa kurusha midahalo, wakiyaona kuwa yasiyo na thamani mambo ambayo mababu waliyathamini, na kufikiria viwango vya Kigiriki kuwa bora.*” (**The Bible, An American Translation, Smith-Goodspeed** version).

Uyahudi wa siku za kisasa unatafuta kuelezea, katika njia nyingi tofauti vifuniko vya vichwa wanavyotumia kwa ibada yao. Yamekuwa maoni ya mwandishi kwamba maelezo tu ya busara kwa vazi la kichwa linalotumika kwa sasa, yanarudisha nyuma kwa zama za Makabayo wakati mazoea ya kimaandiko ya watu Wayahudi yalishawishiwa na jeshi la makazi la Kigiriki chini ya Antiokia Epifanesi. Hakuna rekodi yoyote kwamba Yahshua aliye Messiah alifunika kichwa chake kwa ibada wakati alipokuwa hapa duniani. Mtume Paulo anashindana kwa nguvu kwamba MWANAMUME lazima awe na kichwa chake KIMEFUNULIWA kwa ibada, wakati kichwa cha MWANAMKE KIMEFUNIKWA kwa sababu mwanamume na mwanamke wanaonyesha ukichwa wa kiroho. (1 Wakorintho 11:2-16). Umeweza kusoma nakala yetu ya bure yenye mada UKICHWA? Kama hapana, andika kwa hiyo mara moja. Marabi wengi watathibitisha kwamba hakuna amri ya kibiblia kwa mwanamume kuweka kichwa chake kimefunikwa kwa ibada- hiyo ni mila tu.

Kama ulivyoona tayari kutoka kwa **Encyclopedia Britannica**, *mortaboard* ya aina ya kona nne ya kofia ya kitaaluma inafuatilia

*“Na kufanya vijana wazuri zaidi kufaa kofia ya kigriki. Na kwa nguvu hiyo akaendelea kwa mitindo ya Kigriki na kuja kwa desturi geni kukapanda, kwa sababu ya kuzidi kwa uovu kwa Jason [mwenye dhambi], ambaye hakuwa kuhani hata kidogo…”*

Apokripa
2 Makabayo 4:11



kwa uwakilishi wa halo. Watu wa umaarufu, ambao waliaminika kushikilia uhusiano wa karibu na m-ngu jua, waliwakilishwa kama walio na halo kuzunguka vichwa vyao. Makuhani wa sanamu wa Wakanani waliwakilisha muungano wao na jua kupitia *tonsure*, kunyoa vichwa vyao kuacha nywele za mviringo.

Kama **Encyclopedia Britannica** inavyoashiria, halo za mraba, au nimbus, imeweza kubakia leo katika *mortarboard* ya kitaaluma. Utafiti wa kuangazia kuthibitisha hili unaweza kupatikana kwa kusoma **Oxford English Dictionary** chini ya mada "Cap." Sehemu juu ya "cap" inatuelekeza kwa jina *cater*. Jina linalo asili ya mzizi katika neno *quatre*, *robo*, au *nne*. Pia inasemekana kumaanisha *diagonal*.

Neno *catercap* linarejelea kwa *mortarboard* yenye pembe nne pamoja na kofia kwa ambayo inabandikwa, ikielezea kofia ya mraba inayovaliwa na wasomi kwa pembe ya *diagonal*, pointi moja mbele. Mvaliaji wa kofia kama hiyo anatambuliwa kama mtu wa chuo kikuu.

Entimolojia ya kihistoria inatoa nje marejeleo yafuatayo ya fasihi: (1588) *"Wewe msimamizi John Catercap, ni mtu fulani nchini*;" (1589) "*Wao [Bwana Petro na Paulo] hawakuwa yeyote ya haya, Catercap, waliohitimu wala madaktari*;" (1691) "*Hakuogopa hata kuhani mwenye fahari, papa aliye dhidi ya ukristo, Tyrrraneous Prelid, wala catercaps [*mwenye dhambi*]*. Kwa kuongezea, neno cater-capt (kuvalia catercap, kitaaluma) lilitumiwa hivyo katika 1669: "*kasisi mwenye kiburi… na mbaya zaidi kwaa maendeleo dhidi ya mbunge, kama catercap wenzake wote walivyo pia."*

Kwa hivyo, catercap inaashiria mtaalamu na inarudisha nyuma kwa mila za kale za upagani ambapo jua liliabudiwa. Imeainishwa waziwazi kwamba sanaa za mapema katika zama zetu za kawaida hazikuonyesha watu wamevalia halo, kwa sababu hili ni la UPAGANI katika asili, lakini, baada ya uasi unaokua, halo ilionyeshwa kwa mavazi ya kikuhani na *mortarboard* ya kitaaluma.

## Sefania Anaonya Dhidi ya Upagani

Nabii Sefania katika mlango wa kwanza wa unabii wake, anatoa hukumu ya Mwenye-nguvu Yahweh dhidi ya ibada potofu ya upagani. Yahweh anasema, ***"Nitamkomesha mwanadamu na mnyama, nitakomesha ndege wa angani, na samaki wa baharini, na hayo makwazo pamoja na wabaya; nami nitamkatilia mbali mwanadamu, asionekane juu ya uso wa nchi, asema Yahweh."*** (Sefania 1:3).

Yakiambatanishwa kwa ukr-sto wa kawaida ni wingi wa mila za upagani zinazoonyesha ibada ya kale ya jua. Ibada ya Jumapili ni siku ya kawaida ambayo imewekwa kando kwa ibada ya umma. Uwakilishi wa jua, kupitia kwa matumizi mengi ya duara kama ishara na sanaa za kidini inasaliti asili yake. Msalaba ni ishara tofauti ya ibada ya jua iliyotumika sana katika upagani wa kale. Hata neno "Church-kanisa" limeweza kufuatiliwa na Dr. Bullinger katika **The Companion Bible** kwa neno la Kiebrania *kikkar* (mduara au diski), dhahiri likimaanisha tufe la jua. Uwakilishi huu wote unafuatiliwa kwa ibada ya kale ya Misri na Kibabeli na, pengine hatimaye, kwa uasi kabla ya gharika ya Kaini.

Wakati mwandishi alitambua UKWELI huu WA KUSHTUA kwa mara ya kwanza, alishangaa kwamba Mwenye-nguvu Yahweh hajatumia nguvu yake kubwa kuondoa kabisa uchafu huu, uharibifu wa upagani kutoka duniani. Walakini, mawazo yalivutiwa juu yake kwamba katika nyakati za mwisho Yahweh anawaita watu kwa ajili ya Jina Lake. Watu hawa polepole wanaletwa kwenye maarifa ya Ukweli wake safi wa milele. Watumishi wa Yahweh wanahubiri nyama ngumu ya Neno la Yahweh katika juhudi kusafisha kundi hili lililochaguliwa la watu kutoka kwa mazoea yao ya wakati uliopita ya upagani, ili kwamba waweze kutoa ibada safi kwa Mwenye-nguvu Yahweh.

Utaweza kutambua kwamba umuhimu wa uteuzi huu wa mabaki ya Ibada ya Kweli utajitokeza wazi sana katika kifungu kilichonukuliwa cha Sefania, kama vile mlango wa 3, mstari wa 9 na 10. ***"Maana hapo ndipo nitakapowarudishia mataifa lugha iliyo safi, wapate kuliitia jina la Yahweh, wamtumikie kwa nia moja. Maana toka nchi iliyo mbali na mito ya Kushi, waniombao dua, yaani binti za watu wangu waliotawanyika, wataleta matoleo yangu…. Mabaki ya Israeli hawatatenda uovu, wala kusema uongo; wala ulimi wa hadaa hautaonekana kinywani mwao; kwa maana watakula na kulala, wala hapana mtu atakayewaogofya."*** (Sefania 3:9-10, 13). Ni matumaini yetu kwamba kila msomaji atakuwa Mwabudu wa Kweli Mtiifu.

## Yahweh Anahukumu Ibada Iliyoasi ya Baali

Nabii anaelezea sababu kwa hukumu ya Yahweh. ***"Nami nitaunyosha mkono wangu juu ya Yuda, na juu ya watu wote wakaao Yerusalemu; nami nitayakatilia mbali mabaki ya Baali, yasionekane mahali***

*Continued on page 13.*



SEHEMU 7

# Messiah katika Agano la Kale

Na Mzee Jacob O. Meyer

Vipi utajua kwamba umeweza kupokea upatanisho kwa ajili ya dhambi zako katika damu ya Yahshua aliye Messiah? Unaweza kusema kuwa unayo Agano Jipya na kwamba Agano Jipya linafunua kwamba Yahshua aliye Messiah alikuja duniani humu, kwamba alikufa kwa dhambi zetu, na akamwaga damu Yake juu ya mti wa Kalvari, ili kwamba tunaweza kukombolewa kutoka kwa dhambi zetu. Hilo ni kweli kabisa, na ikiwa kwa dhati Ungeuthibitisha ukweli huu, ungekuwa sahihi. Hata hivyo, ni wapi unapata kwamba Yahshua aliye Messiah angekufa kwa ajili ya dhambi za binadamu, na vipi unajua kwamba binadamu hata ni kiumbe mwenye dhambi?

Haya ni maswali mazuri, wakati unaketi chini na kuyazingatia. Sababu kwa nini ninauliza maswali haya na kuyawasilisha kwako ni kukuchochea kufikiria kwako.

Unajua kwamba watu wengi leo wanataka kutenganisha, au kugawanya kati, Agano la Kale na Jipya? Unajua kwamba wao ni wasio na haki kufanya hivyo? Watu ambao wanagawanya Biblia kati ya Agano la Kale na Jipya wanafanya hivyo bila ya kuhesabiwa haki. Je, unatambua kwamba hakuwezi kupatikana Maandishi katika Biblia ambayo yanaonyesha lazima tuwahi kutenganisha kati ya Agano la Kale na Jipya, au

kwamba tunaruhusiwa kufanya hivyo?

Bila shaka, mtu ni kiumbe mwenye dhambi. Kila mmoja wa kabila ya binadamu, ambaye ameweza kuzaliwa tangu Adamu na hawa, anatangazwa kuwa mwenye dhambi. Vipi unajua kwamba wao ni wenye dhambi? Dhambi ni nini? Dhambi ni uasi wa Sheria ya Yahweh (1 Yohana 3:4). Wakati mtu anafanya dhambi na kuasi (kukiuka) Sheria za Yahweh, basi anaanguka chini ya adhabu kwa dhambi. Kama dhambi ni uasi wa sheria ya Yahweh, basi lazima afe kwa dhambi zake, kwa sababu kifo (kuuawa) ni adhabu kwa dhambi (Warumi 6:23)

Mwenye-nguvu Yahweh katika kipindi cha Bustani la Edeni, alitoa sadaka baadhi ya wanyama alipofanya kanzu kwa Adamu na Hawa. Alimwaga damu ya wanyama wasio na hatia kwa sadaka mbadala na kuwavisha Adamu na Hawa ngozi zao. Hili lilikuwa utangulizi wa Yahshua aliye messiah na sadaka Yake. Kama jambo la kweli, hata kabla ya Mwenye-nguvu kutoa sadaka wanyama hao, alifanya unabii kwa Adamu na Hawa kwamba hatimaye mbegu ya mwanamke ingeweza kukiponda kichwa cha nyoka. Mbegu hiyo ya mwanamke inarejelea haswa kwa Yahshua aliye Messiah. Iliashiria moja kwa moja kuelekea kwa sadaka ya Yahshua juu ya mti wa Kalvari.

Tunaichukulia Biblia kwa urahisi sana wakati mwingi! Biblia inayo majibu kwa maswali yetu. Yote tunahitaji kufanya kuendeleza imani ni kuchimbua nje majibu. Mwenye-nguvu Yahweh aliwaaongoza manabi Wake katika Maandishi ya Agano la Kale kuweka chini baadhi ya unabii huu. Aliwaongoza manabi kuandika vitabu vyao vya kinabi ili kwamba tungeweza kujitayarisha sisi wenyewe dhidi ya wakati mbaya unaokuja katika mwisho wa zama. Aliwahamasisha ili kwamba tunaweza kuhakikishiwa kwamba, wakati alimtuma Messiah duniani humu, mtu binafsi sahihi angeweza kutambuliwa kama Messiah na angekubaliwa na watu Wake.

Ndio, Yahshua aliye Messiah ni Mfalme wa kweli, aliyetiwa mafuta na Yahweh. Hata hivyo, ni watu wangapi kwa kweli wameikubali sadaka Yake? Wanataka dini bila damu, lakini, kinyume chake, Biblia inazungumza kuhusu dini ya damu. Ama mtu binafsi afe kwa dhambi yake mwenyewe, au inahitaji kifo cha mbadala. Yahshua aliye Messiah alinuiwa kuwa sadaka hiyo ya mbadala kwa binadamu.

Ruhusu tusome kutoka mlango wa 53 wa Isaya, ambapo maelezo wazi ya Yahshua aliye Messiah yanaonekana. Huu ni unabii ambao kwa kawaida unapuuzwa na wachanganuzi wa kidini. Nimeweza kuambiwa na Wayahudi mbalimbali kwamba kifungu hiki kamwe hakisomwi katika huduma ya sinagogi. Walakini, kinaonyesha kwa wazi kwamba Yahshua ni Messiah wetu, na kinatabiri kwamba angekuja na kufa kwa dhambi ya watu Wake.

Isaya 53 inaanza **"Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa Yahweh amefunuliwa nani?"** Kifungu hiki cha Maandiko katika mstari wa 1 kilinukuliwa katika mahali mbalimbali katika Agano Jipya. Kwa mfano, kilinukuliwa katika Yohana 12:38 na Warumi 10:16. Wote Mtume Yohana na Mtume Paulo wananukuu mstari huu katika Agano Jipya.

Kitukio, kama hujawahi kuijua, kunazo takribani nukuu 287 katika Agano Jipya ambazo zinanukuliwa moja kwa moja kutoka kwa Agano la Kale. Zilinukuliwa neno moja kwa moja katika Agano Jipya. Kunavyo vifungu vingi zaidi vya Agano la Kale vinavyodokezwa katika Maandishi ya Agano Jipya. Huu ni ufunuo kabisa unapofikiria kuuhusu, kwa sababu waandishi wa Agano Jipya hawakuwa wanaandika kitabu kipya. Walikuwa tu wanaandika **nyongeza** kwa Maandiko ya Agano la Kale.

Unajua ni wapi Agano Mpya linapatikana kwanza katika Biblia? Agano mpya kwa kweli linapatikana katika Agano la Kale katika Yeremia 31:31-34. Kwa sababu tu Agano mpya inaitwa 'Mpya' haimaanishi kwamba haikutajwa kwanza katika Agano la Kale. Kumbuka, neno, "Agano la Kale na Jipya" kwa kweli, ni lenye matatizo na kibinafsi.

***Alikuwa mzizi kutoka kwa ardhi iliyokauka ya nasaba ya Daudi. Hakuwa na vipengee vyovyote vya urembo ambavyo vingewavutia watu kwa asili. Ujumbe Wake ungezungumza kwa niamba Yake. Alikuwa mtu wa huzuni na ajuaye sikitiko, na watu walificha nyuso zao kutoka Kwake.***

Unabii wa Isaya mlango wa 53 unaanza, ***"Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta?"***Ni watu wangapi kweli wanaamini?

Kuendelea na mstari wa 2, ***"Maana alikua mbele zake kama mche mwororo, na kama mzizi katika nchi kavu; yeye hana umbo wala uzuri; hata***

***tumtamani tunapomwona. Alidharauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu."***

Hasa kama kifungu hiki kinaelezea, Yahshua alitimiza unabii huu wote wakati alitembea dunaini, katika wakati alipokuwa anawafundisha Israeli na wakati alifanya kuonekana Kwake, alikuwa akileta Neno la Yahweh kwa umakini wa wasikilizaji Wake. Ndio, hakuwa na mwili mzuri; hakuwa mtanashati- aina ya mwigazaji wa sinema. Alikuwa Myahudi wa kawaida wakati alitembea duniani. Alionekana kabisa kama watu wa Yudea. Alikuwa mzizi kutoka kwa ardhi iliyokauka ya nasaba ya Daudi. Hakuwa na vipengee vyovyote vya urembo ambavyo vingewavutia watu kwa asili. Ujumbe Wake ungezungumza kwa niamba yake. Alikuwa mtu wa huzuni na ajuaye sikitiko, na watu walificha nyuso zao kutoka Kwake.

Hivyo, wengi wa watu maarufu wa dini wa siku Zake hawakumkubalia yeye. Walimkataa Yeye, kwa sababu hawakuelewa unabii huu ambao alikuwa anatimiza hasa machoni mwao kabisa. Ni watu wangapi leo wanatambua kwamba wanasimama kwenye ukingo wa Dhiki na hawana wasiwasi? Hawaelewi unabii ambao uko katika Biblia unaohusiana kwa nini iliyo mbele. Wakati ulio mbele utakuwa wakati wa uovu mkuu, wa mtikisiko na dhiki katika mwisho wa zama.

Bila shaka, watu wengi katika Ukr-sto wa kawaida wangesema, 'Naam, kama ningekuwa nikiishi katika wakati wa Yahshua, ningeweza kumkubali. Ningeweza kuwa mmoja wa wanafunzi Wake. Ningeweza kumfuata Yeye kila mahali.'Lakini hilo ni vigumu lingekuwa ndilo tukio, kwani watu hao haswa hawatii ujumbe Wake leo! Wanaonekana kutaka kuwa na keki yao na kuila pia. Wanataka maarifa ya Messiah, lakini hawataki kumpa Yeye muamana kwa ujumbe ambao kwa kweli aliuhubiri. Wanayo bidii ya Yahweh, lakini sio kulingana kwa maarifa, kama tunavyosoma katika Warumi 3:2.

Basi tuendele kusoma kwa Isaya 53:4, ***"Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tilimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Elohim, na kuteswa."*** Hapa katika kifungu, tunawasili kwa sehemu kubwa ya maarifa. Neno linatuambia sisi kwamba alikuwa Yahweh Mwenyewe aliyemtoa Mwana aweza kupigwa na kuteswa. Angeweza tu kuliondoa taifa la binadamu katika hukumu kwa dhambi na kuanzia na aina nyingine ya watu, lakini alitaka asichukue mwelekeo huo. Alimpa binadamu aliyepotea nafasi kuokolewa kwa kumtuma Mwana Wake kuwa Mwokozi wa ulimwengu. Angalia 1 Yohana 4:14.

Upendo gani Yahweh alionyesha kwa wanadamu! ***"Kwa maana jinsi hii Yahweh aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Elohim hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye."***(Yohana 3:16-17).

Tambua mstari wa 5, ***"Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichumbuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona."***Neno kujeruhiwa hapa lina maana ya kuchoma. Katika Kiebrania, ni *mecholal*, na lina maana *kutia(kuchoma) kupitia*.

Katika kitabu cha Nabii Zakaria, mlango wa 12, mstari wa 10, tunasoma, ***"Nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwomboleza, kama vile mtu amwombolezavyo mwanawe wa pekee…."*** Hivi ni vifungu viwili vya maandiko (unabii mara mbili) ulioelekezwa kwa kifo cha Yahshua aliye Messiah, ambaye angetolewa kama Mwana-kondoo wa Yahweh wa sadaka kuokoa ulimwengu kutoka kwa dhambi zake. Kifo chake kilitukomboa sisi kutoka kwa hali yetu iliyopotea na damu yake iliyomwagika ilifidia kwa dhambi zetu.

Ruhusu tusome mstari tena ***"Bali alijeruhiwa [alichomwa] kwa makosa yetu…*** Neno *makosa* hapa linamaanisha k*uasi au uasi*."***Alichumbuliwa kwa maovu yetu."***Neno *maovu* linamaanisha *kuinama* au *isiyonyooka*. Kwa sababu hiyo, tunaweza kutafsiri kifungu hiki kama ifuatavyo:Bali alijeruhiwa kwa kuasi au uasi wetu. Alichumbuliwa kwa kuinama au kutonyooka kwetu. "***Adhabu*** [kichapo au adhabu] ***ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona***."

Naam, Yahshua Mwana wa Yahweh, alichukua adhabu yetu juu yake, na kujitoa Mwenyewe kama mwanakondoo wa Yahweh, wa sadaka anayechukua dhambi za ulimwengu.

Katika mstari wa 7 na 8 tunasoma, ***"Alionewa, lakini alinyenyekea, wala hakufunua kinywa chake; kama mwanakondoo apelekwaye machinjoni, na kama vile kondoo anyamazavyo, mbele yao wakataao manyoya yake; naam, hakufunua kinywa chake. Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa; na kwa kizazi chake ni nani mwiongoni***


***mwao alizingatia kwamba, amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu?”*** Yahshua alijitoa Mwenyewe kama mwanakondoo wa sadaka ya dhabihu juu ya mti wa Kalvari. Pigo la hukumu, au adhabu, ilikuwa inayotufaa kama wenye dhambi. Mshahara wa dhambi ni mauti (Warumi 6:23). Walakini, Yahshau aliye Messiah alichukua adhabu yetu juu yake Mwenyewe.

Katika mstari wa 9 tunasoma, ***“Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; na pamoja na mtu tajiri katika kufa kwake; ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake.”*** Unabii unathibitisha kwamba angekuwa asiye na dhambi, na bado, aliangamizwa kwa sababu ya dhambi za watu Wake. Aliwekwa kwenye kaburi la Yusufu wa Arimathea, mtu aliyekuwa tajiri sana, na akatimiza unabii huo pia. Kisha, alifufuka tena kutoka kwa kifo na kaburi katika siku ya tatu, ili kwamba tuweze pia kuwa na imani na tumaini katika ufufuo. Unayo imani na tumaini katika ufufuo?

Tunataka kukusaidia kufikia kwa imani hiyo na tumaini katika ufufuo na katika siku zijazo uzima wa milele katika ufalme wa Yahweh.

Tunakualika wewe kuandika kwa baadhi ya maandishi yetu ya bure juu ya kutundikwa kwa Messiah na ishara ya Umessiah Wake, siku tatu na kucha tatu alipokuwa kaburini. Andikia kwa Assemblies of Yahweh, Po Box C, Bethel, PA 19507.

Kwa nini usiwasiliane mara kwa mara na Assemblies of Yahweh? Tungependa kukupa wewe zawadi ya maarifa bure, kama tu Yahweh alivyotoa Baraka hii kwetu. SNB



# Kofia & Gauni

## YA KUHITIMU



*Continued from page 9.*

***hapa, na hilo jina la Wakemari pamoja na makuhani.”*** (Sefania 1:4).

Kama tulivyoona tayari, Yerusalemu, kituo cha ibada safi ya Yahweh kwa ulimwengu huu wote, kilikuwa kilichoharibika katika wakati wa Mfalme Suleimani. Suleimani alikuwa ameingiza ibada ya upagani Yerusalemu kupitia dini za umati wa wake zake na Masuria.





**Kuhani wa Orthodoksi ya Ugiriki huko Yerusalemu, kwenye Ch-rch of the Holy Sepulchre.**

Inaonekana kama kwamba kila mmoja wa wanawake hawa alileta ibada yake aliyoipenda binafsi pamoja naye, 1 Wafalme 11:1-10. Madhabahu zilijengwa katika bonde la Hinomu kwa kila mmoja wa wanawake hawa wa kigeni. Kila hekalu ya uabudu wa sanamu ilisimamiwa na makuhani walioingizwa wa upagani. Inavyoonekana baadhi ya makuhani hawa walikuwa wanafalsafa wenye uwezo, kwa sababu inaonekana kama kwamba kwa njia fulani walimshawishi Mfalme Suleimani kwamba ulimwengu wote ulikuwa unamwabudu Aliye na Nguvu Mmoja- kwa njia tofauti tu. Hili linaweza kuwa sababu kwa nini Suleimani alidhoofika katika uamuzi wake kumtumikia Mwenye-nguvu Yahweh peke yake, mpaka hatimaye, katika mwishoni mwa maisha yake, Yahweh alikuwa mwenye hasira na yeye kwa uasi wake.

Mwenye-nguvu Yahweh anatangaza kwa nguvu kwamba ataondoa makuhani wa sanamu za upagani na mabaki ya Baali kutoka Yerusalemu. Baada ya siku yake kuu ya hukumu katika mwisho wa zama, ibada safi ya Yahweh itarejeshwa katika Yerusalemu. Kwa sababu hii, Mwenye-nguvu Yahweh, leo, anatayarisha mabaki Yake ya watoto wa kiroho kwa kusudi hili la kuwafundisha watu wa ulimwengu huu ibada safi,iliyorejeshwa, ya Aliye na Nguvu wa Kweli wa Israeli, Mwenye-nguvu Yahweh, na Mwana Wake, Yahshua aliye Messiah.

## Desturi za Kuabudu Sanamu Zilizochukuliwa na Israeli

Nabii Sefania anaelezea baadhi ya mila za machukizo za makuhani hawa wa sanamu wa Baali. ***"Na wale walisudiao jeshi la mbinguni juu ya dari za nyumba; na hao waabuduo, waapao kwa Yahweh na kuapa pia kwa Malkamu; na hao waliorudi nyuma, na kuacha kumfuata Yahweh; na hao wasiomtafuta Yahweh, wala kumwulizia.***

***"Nyamaza kimya mbele za Mwenye-enzi Yahweh; kwa maana siku ya Yahweh I karibu; kwa kuwa Yahweh ameweka tayari dhabihu, amewatakasa wageni wake. Na itakuwa, katika siku ile ya dhabihu ya Yahweh, nitawaadhibu wakuu, na wana wa mfalme, na watu wote waliovaa mavazi ya kigeni. Na katika siku ile nitawaadhibu hao wote warukao juu ya kizingiti, waijazao nyumba ya Mwenye-enzi wao udhalimu na udanganyifu. Na katika siku ile, asema Yahweh kutakuwako sauti ya kilio kutoka lango la samaki, na mlio mkuu katika mtaa wa pili, na mshindo mkuu kutoka milimani. Haya! Lieni, ninyi mkaao katika Makteshi, maana wafanya biashara wote wameangamia; hao wote waliokuwa na mizigo ya fedha wamekataliwa mbali. Kisha itakuwa wakati ule nitauchunguza Yerusalemu kwa taa; nami nitawaadhibu watu walioganda juu ya sira zao; wasemao katika mioyo yao, Yahweh hatatenda mema, wala hatatenda mabaya. Na huo utajiri wao utakuwa mateka na nyumba zao zitakuwa ukiwa; naam, watajenga nyumba, lakini hawatakaa ndani yake; nao watapanda mizabibu, lakini hawatakunywa divai yake."*** (Sefania 1:5-13).

Tunaweza kutambua wale ambao wanainama juu ya paa za nyumba na kuabudu jeshi la nyota kama wale ambao wanajihusisha kwa unajimu, urudishaji nyuma kwa vitendo maarufu katika mnara wa Babeli. Mwenye-nguvu anaonya kwamba watu hawawezi kupanda uzio katika maoni yao ya kidini, au kuruka nyuma na mbele kutoka dini moja hadi nyingine,



**Nguo nyeusi na mavazi mengine ya upagani yanayovaliwa na makuhani waabudu sanamu.**

au fundisho moja la kidini hadi nyingine, kama alivyofanya Israeli katika 1 Wafalme 18. Lazima wafanye uamuzi imara kati ya Yahweh na Baali (akiwakilishwa na Moleku). Yahweh atawaadhibu wale ambao wanavalia katika mavazi ya kigeni (pengine marejeleo kwa mavazi ya Kibabeli ya Yahshua (Joshua) 7:21, au vazi la upagani *kemarim*). Mavazi hayo ya kigeni yanahusiana kwa nguo nyeusi na mavazi mengine ya upagani yanayovaliwa na makuhani wa sanamu. Kwa nini mwanamume Muisraeli Akani alitamani Upagani kama huo? Umewahi kumwona yeyote akiepuka kukanyanga kizingiti? Hili linarejelea kwa ibada ya Dagoni (1 Wamueli 5). Makuhani wa Dagoni waliepuka kukanyanga

**Plasterer na chokaa.**



kizingiti wanapoingia nyumba za ibada. Ibada yao ya sanamu imekuwa na uwajibikaji kwa kuijaza dunia hii na vurugu. Mwenye-nguvu Yahweh anasema lazima tuondoe hilo ambalo halifurahishi Kwake. Mwandishi aliweza wakati mmoja kutolewa zawadi ya $ 100 kwa picha ya kuhani wa Katoliki akikanyanga kizingiti.

*Catercap* inaweza kuwa imewakilishwa katika mstari wa 10 wa Sefania 1, ambapo **New International Version** inatafsiri "New Quarter." Pengine muungano unajitokeza pia katika mstari wa 11, ambapo neno MORTAR linapatikana katika Kiebrania. Baadhi ya watoa maoni wanaamini kwamba neno linalohusiana kwa chokaa na mchi zilizotumika kutayarisha vitu mbalimbali. Pengine ilihusiana kwa umbo la kijiografia la eneo lakini pia inaweza kurejelea kwa *mortarboard* ya kale inayotumika kwa sasa katika kazi mbalimbali za ujenzi na pia kutumika katika sherehe mbalimbali za siku za kisasa za kitaaluma.

Hukumu ya Yahweh kwa wazi inaonyeshwa katika Sefania 1:18 ***"Fedha yao wala dhahabu yao havitaweza kuwaokoa katika siku ile ya ghadhabu ya Yahweh; bali nchi yote pia itateketezwa kwa moto wa wivu wake; maana atawakomesha watu wote wakaao katika nchi hii, naam, ukomo wa kutisha."***


Kutoka kwa vifungu hivi vya kinabii vya kibiblia ambavyo tumeweza kuchunguza, inakuwa wazi dhahiri kwamba Mwenyenguvu Yahweh analaani kwa nguvu sana wale ambao wanajiita wenyewe Waabudu wa Kweli wakati wanafuata mila za waabudu wa sanamu za upagani. Yahshua anatuambia kwamba lazima tuwe kamili katika huduma yetu ya kujitolea kwa Aliye Juu, Mathayo 5:48. Lazima tutumie maarifa haya ya kimaandiko kwetu wenyewe na kuishi Kwake. Lazima pia tuelewe kwamba ni wajibu juu yetu kurejesha njia za zamani ambapo ipo nji nzuri na kutembea ndani yake, Yeremia 6:16. Hatuwezi kupokea Baraka kutoka kwa Aliye Juu mpaka tuonyeshe utiifu wa unyenyekevu Kwake na Sheria Zake.

## Hekima ya Yahweh Iliyokataliwa na Ulimwengu

Kusanyiko la Kitume la kitabu cha Matendo ya Mitume walionyesha maarifa yao na ufahamu wa neno la Yahweh. Yahshua aliye Messiah alikuwa amewafundisha wanafunzi Wake kwa miaka mitatu na nusu na kufikisha kwao maarifa ya milele ambayo yanapita dhana za ufahamu za binadamu. Ni iliyo bora zaidi kwa maarifa ya ulimwengu. Maarifa yaliyoshikiliwa na ulimwengu yatajumuisha na kuiga baadhi ya hekima ya Yahweh,lakini katika uchambuzi wa mwisho, Roho Mtakatifu utafunua maarifa ya kina zaidi kuliko elimu ya kudunia inayofunza, na hapo hekima ya wenye busara itakuwa kama upumbavu (1 Wakorintho 3:18-20).

Hili linaonyeshwa wazi kabisa katika Matendo ya Mitume 4:13. ***" Basi walipoona ujasiri wa Petro na Yohana, na kuwajua ya kuwa ni watu wasio na elimu, wasio na maarifa, wakastaajabu, wakawatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yahshua."***

Wanafunzi wa Yahshua waliitwa wanaume wajinga na wasio na elimu. Tayari taasisi za kidunia za Uyahudi walikuwa wameingiza dhana mingi za mataifa




kwenye mfumo wao wa kikanisa. Yahshua aliye Messiah alikuja kuondoa maarifa yaliyoharibika ya binadamu na mila, akihimiza kubadilishwa kwayo na hekima ya kweli, safi inayofundishwa na Roho Mtakatifu, maarifa, na ufahamu ambao unapatikana katika Maandiko Matakatifu, kama yanavyofunzwa na Mwenye-nguvu Yahweh, Baba wetu wa mbinguni. Yahshua ni mwalimu mkuu zaidi aliyewahi kutembea duniani. Anajulikana kama Rabi wa Kiyahudi, lakini asiyehusishwa na Yeshivoth (vyuo vikuu) maarufu vya Hillel na Shemai.

Maarifa sahihi ni nini? Je, hayapatikani katika Maandiko Matakatifu? Maarifa ya kidunia yanaweza kuwekwa kiwango kilicho bora juu ya yale ambayo watumishi wa Yahweh wanafundisha? Ni nadra kwa ulimwengu kutambua hati ya utambulisho wao, ingawa wanafunza usafi wa Neno la Yahweh- shauri zima la Neno la Yahweh.

Petro na Yohana hawakuwa na ubaguzi. Walikataliwa na Sanhedrin. Waliitwa wajinga na wasio na elimu. Hata hivyo, hekima yao ilikuwa ya juu zaidi kwa mbali ya mafundisho ya kikanisa ya wakati wao. Hili lilionyeshwa kwa majibu waliyotoa kwa waulizaji wao. Tunapaswa kudharau yale Roho Mtakatifu unafunua leo kupitia watumishi wa kweli wa Yahweh? Yahshua ndiye Kichwa cha Mwili na anawafunza wasemaji Wake hekima ambayo inawachanganya wenye hekima wa kidunia. (Luka 2:41-52).

### Hitimisho

Katika nakala hii ya utafiti, mhariri ameweka nje baadhi ya sababu kwa nini washiriki wa Assemblies of Yahweh hawajiviki wenyewe katika mavazi ya kielimu ya sherehe wanaposhiriki katika sherehe katika uwanja wa kielimu wa kidunia. Habari tuliyowasilisha inakuja kutoka kwa baadhi ya nyenzo za utafiti zinazozingatiwa sana katika ulimwengu wa kielimu, **Encyclopedia Britannica** na **Oxford English Dictionary.** Assemblies of Yahweh inaweka thamani kubwa juu ya elimu, na baadhi ya elimu hiyo inafundishwa na mfumo wa kielimu wa dunia. Walakini, lazima tukatae wazi vitendo ambavyo vinafuatiliwa kwa mazoea ya kale ya upagani. Yote ya ambayo tunamini na kuweka vitendoni lazima yawe katika maelewano kamili na Neno la Yahweh. Kwa hivyo, Assemblies of Yahweh imeanzisha taasisi yake yenyewe ya kielimu kufunza mafundisho yaliyosafishwa.

Kwa habari hii ya kushangaza tuliyowasilisha, msomaji ana changamoto kuthibitisha kwake mwenyewe ukweli wa hitimisho tulizoweka. Lazima ufanye maamuzi yako mwenyewe. Lazima kibinafsi usimame mbele ya kiti cha hukumu cha Messiah kujibu kwa yale uliyofanya wakati wa maisha yako ya binadamu.

***"Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia Yahweh, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; kwamba ni elohim zile ambazo baba zenu walizitumikia ng'ambo ya Mto, au kwamba ni elohim ya Waamori ambao mnakaa katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Yahweh."*** (Yahshua 24:15).

Kama tu Yahshua, washiriki wa Assemblies of Yahweh kwa hiari wamechagua kumtumikia Mwenye-nguvu Yahweh, na Yeye pekee. Na uweze kuendeleza imani sawa ya kibinafsi. Lazima tumtumikie Yahweh badala ya binadamu. (Matendo ya mitume 5:29). SNB



# Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa

SEHEMU 7


**Na Mzee Jacob O. Meyer**

Katika harakati yetu kufikia Ufalme wa Yahweh, ni muhimu kwamba kila siku tujifunze ukweli wa kina ambao upo katika Maandiko Matakatifu. Kwa sababu hiyo, programu za Jina Takatifu zimeundwa kama programu za kutafiti Biblia, sio programu za burudani. Leo, dini imekuwa hasa sekta ya burudani. Sababu kwa nini hili limefanyika ni kwa sababu watu wanapenda kuburudishwa. Wanapendelea muziki wa kusisimua na mafundisho ya juujuu ambayo hayawahitaji kubadilika kutoka kwa njia zao za dhambi. Walakini, programu za Jina Takatifu sio programu za burudani na zimeweza kuundwa hivyo ili kwamba, baada ya kusikia kwa somo, unaweza kusema kwamba umejifunza kitu fulani kuhusu Biblia, kukuruhusu wewe kukua katika Roho Mtakatifu wa Yahweh na Ukweli.

Umewahi kuzingatia mada ya Sabato? Sikulelewa kama mtunzaji wa Sabato, lakini kama natafiti, ilibidi nikabiliane na ukweli na kufanya uchambuzi wa mada hii muhimu katika Maandiko Matakatifu. Je, sabato iko katika siku ya saba ya wiki, au imebadilishwa ili kwamba Waabudu wa Kweli wanaweza kuabudu katika siku ya kwanza ya wiki? Iliweza kubadilishwa kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza ya wiki wakati Messiah alikufa?

Ilibidi nithibitishe maswali haya yote kwangu mwenyewe, na ninatumai kwamba utafanya hilo pia. Nilijifunza katika Biblia kwamba kupata wokovu, lazima niamue kuishi kwa kila Neno ambalo linatoka kinywani mwa Yahweh. Kama hujawahi kuthibitisha baadhi ya mambo haya, ningependa kukusaidia kuthibitisha mafundisho safi ya Neno la Yahweh.

Yahshua aliye Messiah kamwe hakubatilisha Sheria alipokufa.




Unaweza kuthibitisha hili kwako mwenyewe kutoka Mathayo 5:17-20, Mahubiri ya Yahshua juu ya Mlima. ***"Msidhani ya kuwa nilikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amini, nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie. Basi mtu ye yote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni. Maana nawaambia ya kwamba, haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni."***

Yahshua alikuja na kupitia maisha yake ya haki, aliimarisha sheria, kutoa kwetu mfano wa jinsi lazima tuishi kuwa wanaompenda Baba wetu wa Mbinguni Yahweh. Mafundisho hayo yote ya Maandiko Matakatifu lazima yatiiwe na kutumika kwa maisha yetu ya kila siku.

Tumekuwa tukijadili madarasa manne ya viumbe vilivyoumbwa ambavyo Mwenye-nguvu Yahweh aliumba kuwa watumishi Wake. Madarasa ambayo tumejadili kufikia sasa ni *makerubi*, *maserafi*, na *malachim*. Ningependa kugeuza umakini wetu kwa darasa la mwisho la viumbe vilivyoumbwa- jamii ya wanadamu, hiyo ni, Adamu. Darasa hili la mwisho ni *homo sapiens*, binadamu. Katika Biblia ya Kiebrania, neno Adamu linatumika kama neno la jumla kwa binadamu. Neno *Adamu* linahusiana kwa neno la Kiebrania kwa *udongo* au *ardhi*, ambayo ni *Adamah*, na ina maana ya udongo mwekundu wa nchi takatifu kutoka kwa ambayo Mwenye-nguvu Yahweh alimuumba Adamu. Alichukua mavumbi ya nchi, akileta udongo mwekundu (terra rosa) pamoja na, kuufinyanga aliumba binadamu. Kwenye pua la kiumbe hiki alichoumba, alipuliza pumzi ya uhai. Ninapenda kuirejelea kama Yahweh anatoa kwa Adamu *artificial resuscitation*(ufufuo wa bandia) wa kwanza uliorekodiwa. Elohim alijaza mapafu yake kwa hewa, na Adamu akaanza kupumua, kuwa nafsi hai. Baada ya kumuumba Adamu, aliona hitaji la kuumba msaidizi anayefaa kwa mwanamume na akamuumba Hawa. ***"Yahweh Elohim akasema, Si vema huyu mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye."*** (Mwanzo 2:18). Tambua kwamba neno SI MSAIDIZI(*help mate*), lakini MSAIDIZI ANAYEFAA KWA MWANAMUME.

Kuweka sauti kwa utafiti huu, ningependa tuweze kusoma Zaburi 8:4. ***"Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu*** [Neno hili pia linatafsiriwa kama malaika katika baadhi ya toleo]***hata umwangalie? Kwa maana umemfanya mdogo punde kuliko Elohim*** [neno hili pia limetafsiriwa kama malaika katika baadhi ya toleo]. Elohim ni roho. Yeye ni aliyeundwa kwa roho isiyoonekana, na ambao wanamwabudu Yeye lazima wamwabudu Yeye katika Roho na katika Ukweli. Malaika pia waliumbwa chini kidogo kuliko Elohim, lakini malaika bado wako juu yetu (wanadamu), kwa sababu wanayo nguvu zaidi kuliko walivyo binadamu. ***"Umemvika taji ya utukufu na heshima...."***

Ni utukufu gani tulio nao zaidi ya kujulikana kama wana wa Aliye

Juu na siku fulani kubadilishwa kwenye roho katika ufufuo wa wenye haki? Ni heshima gani kubwa Yahweh angetoa kwa binadamu kuliko hiyo? ***"Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umevitia vitu vyote chini ya miguu yake. Kondoo, na ng'ombe wote pia; naam, na wanyama wa kondeni. Ndege wa angani, na samaki wa baharini, na kila kipitacho njia za baharini. Wewe, Yahweh, Mwenye-enzi wetu, jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote!"***

Ningependa kuzingatia kwa programu kadhaa juu ya swali, "***Mtu ni kitu gani***?" na kutafuta kujibu swali hilo kwa kuangalia kwa kina kwenye Neno la Yahweh. Tunapogeuka kwa mlango wa kwanza wa kitabu cha Ufunuo tunapata hapo uumbaji wa binadamu. Yahweh alifanya mbingu na nchi. Mimi si muumini katika mageuzi (evolution). Tunashughulika hapa na Kiumbe wa milele, ambaye hajafungwa kwa wakati. Jina la Mwenye-nguvu linafafanuliwa kama *umilele*, *kuwepo binafsi*, *kuishi milele*. Mzizi wa Jina Yahweh ni kitenzi cha Kiebrania cha kuwepo. Kwa sababu amekuwapo milele, haathiriwi na kipengele cha wakati.

Yahweh anatuambia sisi katika Neno lake kwamba katika siku saba aliumba mbingu na nchi. Kabla ya hayo, *matter* ilikuwepo tayari, na tunaongozwa kuamini (kutoka Isaya 45 na vifungu vingine) kwamba Ibilisi Shetani, dhahiri aligundua njia Yahweh aliyoitumia kushikilia uumbaji pamoja. Hivyo, aliangalia kwa sheria za kiasili za Yahweh. Aliharibu baadhi ya Sheria za Yahweh za uumbaji na mpango wa mambo ukaingia kwenye kinachojulikana katika Kiebrania kama *thehome*, au *shimo*, kutetemeka kwa elementi. Wakati kipengee cha mpango kinaondolewa kwa uumbaji, mkanganyiko unatokea, ambao mtunzi wake ni Shetani. Hili ni dhahiri nini inafanyika wakati Ibilisi Shetani aliweka nje kumdhoofisha Yahweh. Shetani aliurusha uumbaji wenye utukufu wa Yahweh kwenye machafuko.

Basi Yahweh ilibidi azitengeneza upya mbingu na nchi. Vipi tunalijua hili? ***"Bereshith bara elohim eth hashamaim weeth haeretz."*** Soma mstari wa kwanza wa kitabu cha Mwanzo ulionukuliwa moja kwa moja kutoka kwa Kiebrania. ***"Hapo mwanzo*** [kabisa ]***Elohim aliziumba mbingu na nchi.."*** Kisha mstari unaendelea ***"Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu,*** ["*tohu wa vohu*" – maneno *tohu* and *vohu* yanayo maana karibu sawa kihalisi ambayo ni *ukiwa*, *tupu* na *machafuko*]***na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji** [thehome, shimo]* ***roho ya Yahweh ikasonga***[*merechepheth- kukaa, kusonga, brooded]* ***juu ya uso wa maji***[*mayim, kioevu au maji]*.***"***

Elohim basi alianza uumbaji-Wake upya. Kwanza alichunguza machafuko na uharibifu ambao ulikuwa umesababishwa na Ibilisi. Alifanya kitendo dhidi ya machafuko na kuanza kutengeneza upya, kuleta elementi pamoja tena na kuzigeuza kwenye kitu fulani ambacho kingekuwa muhimu. Baada ya hilo, aliujaza ulimwengu na mimea na namna yote ya vitu vinavyomea, na, kisha, akaumba ufalme wa wanyama.

Hatimaye, katika Mwanzo 1:26, ***"Elohim akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi."*** Neno la wanyama ambalo linatumiwa katika nakala ya Kiebrania kwa kweli ni *behemah* katika Kiebrania, na linamaanisha *wanyama wakubwa*. Mtu aliteuliwa kwa kazi yake duniani kusaidia kuifanya ya kuleta mafanikio kama iwezekanavyo.

***"Elohim akaumba mtu kwa mfano wake…"*** Wanatheolojia huria wanataka wewe uamini kwamba Elohim aliumba mtu na uwezo wa kufikiria wa Yahweh pekee, hivyo kuondoa huo umbo wa kimwili wa uhusiano ambao mtu anao na Yahweh. Huwezi sema kwamba Yahweh anao mwili wa kiwiliwili, lakini neno lililotumika linamaanisha kufanana katika fomu. Katika theolojia; mtu anakutana na neno *anthropomorphism*. Anthropomorphism linamaanisha *kumpa Mwenye-nguvu mfano wa umbo la binadamu*. Hili ndilo linaelezewa katika Ezekieli 1:26, ambapo Mwenye-nguvu anaelezewa. ***"Na juu ya mfano huo wa kiti cha enzi, ulikuwako mfano kama kuonekana kwa mfano wa mwanadamu juu yake."*** Naam, Mwenye-nguvu anavyo vidole, pua, macho, na masikio. Binadamu anafanana na Yahweh lakini yeye si nyama na damu kama tulivyo. Yeye ameundwa na nguvu ya roho ya aina fulani. Hatuwezi kwa kweli kutambua nini Roho Mtakatifu alivyo, kwa sababu macho ya binadamu hayawezi kuona roho. Tunaweza tu kuhisi ulimwengu wa roho kwa mioyo yetu na akili. Tunaweza kuona athari ya Roho wa Yahweh kando yetu wakati Yahweh anaondoa vikwazo mbalimbali mbele yetu kupitia miujiza Yake, au maombi yaliyojibiwa.

Ninaamini katika miujiza! Ninaweza kutoa ushuhuda wa kweli leo wa muujiza mmoja kama huo. Bibi yangu aliponywa baada ya mika 60 ya kuishi na vali (valve) ya moyo yenye kasoro. Madaktari wa moyo wawili tofauti walikuwa wamethibitisha kwamba

anayo vali mpya katika moyo wake ambayo inafanya kazi ipasavyo! Madaktari hawa wameniambia moyo ulijiponya wenyewe.Ilibidi nisikubaliane. Moyo haukujiponya wenyewe, kwani mwili wa binadamu huzorota na hauboreshwi kwa wakati. Walakini, muujiza ulitokea kwa sababu ya imani yake na kwa sababu ya nguvu yenye nguvu ya roho wa Mwenyenguvu Yahweh kutenda kazi kwa niaba ya binadamu na kuweka kando mpango wa kiasili wa mambo. Kwa hivyo, nilitaja katika ofisi ya daktari wa moyo wakati mmoja kwamba ninaamini katika miujiza. Nini nilikutana nayo? Ukimya kamili! Watu hawataki kusikia hili.

Ndio, kweli, Elohim alimuumba mtu katika mfano Wake mwenyewe. Tena kumbuka, neno la Kiebrania Elohim limetolewa kwa neno la Kiebrania *uhl* au *eel*, ambalo linamaanisha mwenye-nguvu. Hakuna chochote kilichoharibika sana, au nje ya mahali pake, kwa Yahweh kuponya tunapokuwa na imani sawa kama mababu zetu walivyofanya katika nyakati za kibiblia.

Elohim ndiye Mwenye-nguvu wetu. Yeye ndiye aliye na nguvu kuliko tulivyo na anaweza kuamuru nini tutafanya; kwa hivyo, lazima tumtii yeye. Katika Mwanzo 1, neno Elohim linatumika; walakini katika mwanzo wa mlango wa 2, Jina Yahweh linaonekana. Ninaamini kwamba hakuna tofauti hapa, lakini ni somo ambalo lazima tujifunze. Hakuna hati mbili (hati ya J na ya E) ambazo ziliunganishwa kutengeneza Biblia yetu. Hayo ni mawazo yote ya ubunifu wa wasomi wa mantiki wa Kijerumani. Maandiko Matakatifu yanaunda kitengo kimoja kamili. Nimefanya utafiti wa kina juu ya somo hili na kisha kuingiza ushahidi katika nakala juu ya mada. Kama ungetaka, unaweza kuandika na kuagiza kijitabu hiki chenye mada **Defending Textual Authenticity**. Nimethibitisha makosa ya Graf-Welhausen, nadharia ya hati mbili na umuhimu wa kutambua kwamba Biblia inajumuisha kitengo kimoja kamili. Kijitabu ni bure kwa anayeuliza. Kiombe leo kwa kuandikia Assemblies of Yahweh, Po Box C, Bethel, 19507. Kiombe leo!

Ruhusu tuendele katika Mwanzo 1:27, ***"Elohim akaumba mtu** [Adamu] **kwa mfano wake, kwa mfano wa Elohim*** [umbo, au mfanano wa Elohim ndio tunabeba]***alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba....***" Sio "aliumba yeye kiume na kike"(*zecher unacheva*), lakini badala yake aliwaumba wao, viumbe wawili, mmoja wao kiume na mwingine kike. ***"Elohim akawabariki, Eohim akwaambia, Zaeni, mkaongezeka, mkaijaze nchi, na kuitiisha."*** Neno *kujaza* ni *ma'ale* katika Kiebrania, lina maana ya kujaza. Wakati ninaenda katika Israeli na kuingia kwenye kituo cha petroli, nitasema *ma'ale*( ijaze hadi juu). Yahweh alitangaza kwamba mtu alikuwa "aijaze nchi."

***"Na kuitiisha, mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi. Elohim akasema, tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu, vitakuwa ndivyo vyakula vyenu; na chakula cha kila mnyama wa nchi, na cha kila ndege wa angani, na cha kila kitu kitambaacho juu ya nchi, chenye uhai; majani yote ya miche, ndiyo chakula chenu , ikawa hivyo. Elohim akaona kila kitu alichofanya, na tazama ni chema sana. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya sita."***

Sasa, moja ya mambo ambayo hayaonekani katika tafsiri ya lugha ya Kiingereza ni *Jessive sense*. Elohim alimuumba mtu, lakini maandishi ya Kiebrania yanaonyesha kwamba alibidi Mwenyewe ajitie moyo kumuumba mtu.Kwa nini? Ingawa uchaguzi wa huru umetolewa kwa kila mtu (kila binadamu) duniani, Yahweh alijua kabla ya wakati nini itakayofanyika; hata hivyo, haingilii kati kwa hiari ya mtu. Kila binadamu anahitajika kufanya chaguo lake. Kwa mfano, alihitaji mtu kama Farao, hivyo alimfanya mfalme mwenye kiburi sana kuja kutawala Misri katika wakati wa utumwa wa Waisrali. Wakati Israeli alilia dhidi ya ukandamizaji wa Farao, Yahweh alimtuma Musa kuwatoa watu Wake kutoka Misri. Farao alikuwa na fursa 10 kutubu, kubadilika, na kujitolea mwenyewe kwa mapenzi ya Yahweh; walakini alichagua kutofanya hivyo. Wakati mtu anafanyiza hiari yake katika njia mbaya na kuugeuza mgongo wake kwa njia za Yahweh, unaweza kuwa na uhakika uharibifu wake utafuata.

Je, hiki si kitabu cha kuvutia? Ndio, kweli! Ninafurahia hivyo tu kila wakati ninasoma na kufunza kwa mambo yote ambayo yako katika kitabu hiki cha ajabu kinachoitwa Biblia. Leo tunachimbua vito vya thamani vya maarifa ambavyo vimefichwa hapo kwa muda mrefu.

Hautaendelea kutafiti Neno la Yahweh nasi na kutafuta kukaribia kwa kusanyiko Lake katika nyakati za mwisho? Tunayo maandishi mengi hivyo ya bure ambayo yanapatikana kwako kutumia katika masomo yako kama unatafuta kuwa mtumishi wa kweli wa Yahweh, mtoto Wake mtiifu. Andika kwa Assemblies of Yahweh, PO Box C, Bethel, Pennsylvania 19507. SNB









*Safari ya hivi karibuni ya kihuduma ya Deacon Nathaniel A. Meyer kwenda Ufilipino, Myanmar, na India.*
















*Sacred Name Broadcaster*
*Bethel, PA 19507*

**PERIODICAL**
Reading, PA

# WMLK Radio

## Shortwave ya Assemblies of Yahweh

# Masafa mapya na Nyakati!

**Sasa ikitangaza SIKU SITA KILA WIKI**

**15150 kHz 1200-1700 GMT (8 AM - 1 PM EDT)**

**17525 kHz 1730-2230 GMT (1:30 PM - 6:30 PM EDT)**

**9275 kHz 2300-0400 GMT (7 PM - 12 Midnight EDT)**

**Hewani masaa 24/7 kwa WMLKRadio.com, katika TuneIn.com au Katika station.voscast.com/5cfe89883c143**

(Kumbuka: Kuna wakati ambao WMLK haitangazi kwa sababu ya matengenezo au ukarabati.)

*Kwa Ulimwengu Wote!*